JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)
Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo
Shule ya Sekondari Bagamoyo

Simu ya mkononi: +255 769 397 926

Barua pepe:
bagamoyosecondary@gmail.com
Tovuti:
www.bagamoyo.sc.tz

S. L. P 42

Bagamoyo

Tanzania, East Africa

Kumb.Na.BSS/A.6/36 Tarehe: Mei 2021

……

……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2021/2022

Kwa niaba ya Bodi ya shule, watumishi na wanafunzi wa shule ya sekondari Bagamoyo, ninapenda kuitumia fursa hii kumpongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake kuendelea na masomo ya sekondari na kujiunga na shule hii. **HONGERA SANA.**

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Bagamoyo ipo mkoa wa Pwani wilaya ya Bagamoyo umbali wa takribani km.2.5 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Bagamoyo.

Usafiri wa kufika Bagamoyo unapatikana katika kituo cha mabasi cha Tegeta Nyuki, jijini Dar es salaam. Basi hili litakufikisha Bagamoyo mjini. Kutoka Bagamoyo mjini hadi shule ya sekondari Bagamoyo unaweza kufika kwa mguu au kwa kukodi taxi, bei ni Tshs 4,000/=, kwa kukodi Bajaji Tshs 3,000/= au pikipiki kwa Tshs 1,000/=. Muda wa kuripoti shuleni ni kuanzia **saa 2.00 asubuhi** hadi **saa 10.00 jioni** katika ofisi ya Malezi au ofisi ya mwalimu wa zamu.

MAHITAJI YA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI

Ni vyema mahitaji haya yatimizwe kabla ya kuanza safari ya kuja shuleni.

A**) Malipo:-**

- Karo ya shule ni Tshs. 70,000/= kwa mwaka au Tshs. 35,000/= kwa muhula.
- Fedha kwa ajili ya mchango wa matibabu ni Tshs 10,000/= kwa mwaka au Tshs. 5,000/= kwa muhula.
- Fedha kwa ajili ya kitambulisho ni Tshs 6,000/=
- Ulinzi/wapishi na vibarua Tshs 30,000/= kwa mwaka au Tshs 15,000/= kwa muhula.
- Fedha kwa ajili ya uboreshaji wa taaluma kwa mwaka Tshs 20,000/= au Tshs 10,000/= kwa muhula.
- Mchango wa ukarabati wa Samani za shule Tshs. 15,000/=.
- Mchango kwaajili ya mtihani wa kujipima Tshs.20,000/=
- Fedha ya tahadhari (caution money) Tshs. 5,000/=
- Tshs. 2,000/= kwa ajili ya kuwekewa Nembo ya Shule

Malipo yote yafanyike kwenye akaunti za shule. Shule ina akaunti mbili.

i) **Akaunti ya ada na ulinzi:** Jina la akaunti; Bagamoyo Secondary School.
Namba ya akaunti; A/C 21001200044, Benki ya NMB tawi la Bagamoyo

ii) **Michango mingine;** Jina la Akaunti; Headmaster Bagamoyo Secondary School**.**
Namba ya akaunti; A/C 21001100004 Benki ya NMB tawi la Bagamoyo

Lipa ada na michango mingine katika tawi lolote la Benki ya NMB lililopo jirani nawe ili kuepuka upotevu/wizi wa fedha zako uwapo safarini.

NB: Usiweke fedha binafsi katika akaunti hizo.

Mwanafunzi anashauriwa kuwa na akaunti binafsi ya benki ili aweze kutunza/kutumiwa fedha na mzazi/mlezi wake.

B) I) SARE ZA SHULE; Kwa wavulana:

- Mashati mawili meupe mapya ya mikono mifupi ya kitambaa cha tetroni.
- Viatu vyeusi vya ngozi **soli fupi** vya kupiga rangi na vya **kufunga kwa Kamba**
- Soksi nyeusi jozi mbili.
- Suruali pana za 'dark blue' mbili (2) **zenye marinda mbele**.
- Suruali pana za khaki mbili (2) **zenye marinda mbele**.
- Mkanda mweusi wa ngozi usio na nembo ya kihuni wala bakoli nene.
- Aje na T-shirt ya Blue (maarufu kama Form six) kwa ajili ya kushindia
- Sweta dark blue lenye shingo alama ya V na si vinginevyo

NB: Ataripoti shuleni akiwa amevaa suruali ya 'dark blue' na T-shirt ya Blue. Hairuhusiwi kushona suruali ya kubana na isiyo na marinda (model). Suruali za namna hiyo hazitakiwi kabisa shuleni.

Kwa wasichana:

- Sketi mbili rangi ya Maroon iliyokolea mshono wa rinda box urefu wa sketi ifunike vifundo vya miguu kwa ajili ya sare ya shule.
- Mashati mawili meupe mapya ya mikono mifupi ya kitambaa cha tetroni au nusu kanzu na hijabu nyeupe kwa waislamu.
- Viatu vyeusi vya ngozi soli fupi vya kupiga rangi na vya kufunga kwa kamba au aina ya Juma na Rosa.
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Sketi mbili rangi ya 'Dark blue' iliyokolea mshono wa rinda box urefu wa sketi ifunike vifundo vya miguu kwa ajili ya kushindia.
- Suruali mbili rangi ya "dark blue" zisizobana kwa ajili ya kuvaa usiku kujikinga na mbu wakati wa kujisomea.
- Sweta dark blue lenye shingo alama ya V na si vinginevyo
- Aje na T-shirt ya **blue** (maarufu kama form six) kwa ajili ya kushindia.

NB: Sketi zote ziwe ndefu. Ataripoti shuleni akiwa amevaa sketi ya rangi ya "dark blue" na t-shirt yaBlue. Kwa waislam avae sketi ya "Dark blue"na nusu kanzu ya "Dark blue" na Hijabu ya "Dark blue".

II) SARE ZA MICHEZO KWA WOTE:

- Jezi za rangi nyekundu (t-shirt na bukta)
- Wanafunzi wote waje na viatu vya michezo au raba za michezo

C. MAAGIZO MENGINE YA SHULE

- Cheti cha kuzaliwa na kivuli chake.
- Cheti cha daktari (medical certificate) cha kuthibitisha afya ya mwanafunzi ambayo itajazwa na Hospitali ya Serikali na cheti cha tofauti cha majibu ya vipimo vya TB
- Results slip na kivuli chake.
- Cheti cha kuhitimu kidato cha nne (leaving certificate) halisi na kivuli chake.
- Picha sita (6) za'passport size ziwe na 'background ya blue' na vipimo vya sm.4 kwa 4 na awe amevaa shati jeupe.
- Alete picha moja moja ya passport size za wazazi/walezi wake wawili.
- Sanduku imara la kuhifadhi mali yake binafsi.
- Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe na kijiko (siyo vya plastiki)
- Ndoo ya plastiki yenye ukubwa wa ujazo Lt.10 ya kufulia na kuogea.
- Chombo safi chenye mfuniko kwa ajili ya kuwekea maji ya kunywa.
- Aje na tochi kwa ajili ya tahadhari wakati wa usiku (Isiwe ya kuchaji kwa umeme)
- Bunda mbili za karatasi nyeupe (A4 size) sio za mistari (ruled) kwa mwaka.
- Scientific calculator isipokuwa wanafunzi wa HKL.
- Dissecting kit kwa wanafunzi wa PCB na Dissecting tray kwa wanafunzi wa CBG
- Stop watch kwa wanafunzi wa PCM
- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika. (orodha iimeambatanishwa)
- Mto wa kulalia
- Shuka mbili za rangi moja ya Blue bahari (Light blue).
- Godoro la sponji la futi mbili na nusu (comfy) linapatikana shuleni kwa Tsh. 50,000/= (**Mzazi/mlezi anahiari ya kuja nalo toka sehemu yoyote atakakolipata kwa bei nafuu zaidi**)
- Aje na chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu (**Ni muhimu**)
- Vifaa vya darasani ambavyo ni madaftari (counter books) na mahitaji yote muhimu kadiri ya mchepuo wake.
- Vifaa vya usafi pia vinapatikana shuleni ila **Mzazi/mlezi anahiari ya kuja navyo toka sehemu yoyote vinakopatikana kwa bei nafuu zaidi**.

2. MAHITAJI YA MAKUNDI

ECA	PCB	PCM	CBG	HGE	HKL	EGM
Dawa ya kusafishia vyoo lita tano (LIT)	Slesha		soft broom	soft broom	panga	Mopper Handbroom
	Soft broom	Soft broom	hardbroom	Hard broom		Mfagio wa wima wa chelewa
	Mfagio wa wima wa chelewa	Jembe na mpini	Mfagio wa wima wa chelewa	Mfagio wa wima wa chelewa	Jembe na mpini	

MUHIMU:

i) Mzazi/mlezi unashauriwa kumtimizia mwanao maagizo yote yanayohitajika shuleni na hakikisha kuwa **MWANAO ANAFIKA SHULENI TAREHE ILIYOAGIZWA.**

ii) Kila mzazi/mlezi ahakikishe anatembelea tovuti ya shule (**www.bagamoyo.sc.tz** au www.infotaaluma.co.tz) mara kwa mara ili kuona maendeleo ya mwanae kitaaluma na kimwenendo.

iii) Kila mzazi/mlezi anashauriwa kufika shuleni mara kwa mara katika siku za kazi ili kufuatilia maendeleo ya mwanae kitaaluma na kimwenendo. **Mzazi ataripoti ofisini kila anapofika shuleni.**

iv) Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kuja na nguo au mavazi mengine yasiyo sare ya shule na kuyavaa.

v) Hairuhusiwi kabisa mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo. Kila mzazi/mlezi amtumie mwanae nauli mapema ili kuepuka usumbufu wowote unaoweza kujitokeza.

vi) Mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote na kufanya mitihani na mazoezi kama ratiba ya shule inavyoonesha**.** Utawajibika kufuata sheria zote za shule baada ya kupokelewa shuleni.

viii) **Siku pekee za kutembelea wanafunzi kwa muhula wa kwanza wa masomo ni Jumamosi ya mwisho wa mwezi wa nane na mwezi wa kumi, muhula wa pili ni Jumamosi ya Mwisho ya mwezi wa pili**

ix) **Kila mwanafunzi aweke alama inayoonekana kwenye sare zake na mali zake binafsi**.

Afya ya mwanafunzi:-

Mara upatapo barua hii mwone **Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali** iliyo karibu nawe, ili upimwe kuthibitisha kuwa una afya ya kutosha kusoma masomo ya sekondari. Fomu maalum imeambatanishwa na barua hii. Mara utakapofika shuleni ioneshe ikiwa imejazwa. Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wagonjwa. Hata hivyo ni:-

Ni marufuku kuja na chakula cha aina yoyote hapa shuleni.

Mwanao anatakiwa kutambua kuwa nafasi aliyopata ni nyeti na adhimu hivyo anapaswa kuitumia nafasi hiyo kwa umakini wa hali ya juu ili baadaye aweze kuwa na manufaa kwa familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

Anatakiwa kuripoti shuleni tarehe itakayotangazwa na Wizara, katika ofisi ya malezi baada ya hapo hatapokelewa kwani nafasi yake itachukuliwa na mtu mwingine,yaani siku kumi na nne(14) baada ya tarehe ya kuripoti.

Kwa mara nyingine tena tunampa HONGERA NA KUMKARIBISHA SANA shuleni kwetu.

K. M. MILLONGO
MKUU WA SHULE
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BAGAMOYO
S.L.P. 42
BAGAMOYO

N.B: Tunaambatisha nakala ya sheria za shule kwa ufahamisho kwa mwanafunzi na mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

SHERIA ZA SHULE

Sheria na kanuni za shule zinazingatia msingi ya HEKIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII NA TABIA NJEMA kwa ujumla.

Wanafunzi kwa ujumla wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kwa kauli na vitendo vyao. Hivyo:-

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri.
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi;
   - kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote.
   - Kupeleka au kulia chakula bwenini .
   - Kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele ndefu.
   - Kunyoa kipara.
   - Kutia dawa nywele (curl), na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa.
   - Kuvaa kofia shuleni au mapambo/urembo kama hereni, n.k. akiwa shuleni.
   - Kuvaa viatu vya soli nene au ndefu (ghorofa)
   - Kuvaa kaptula, kandambili na fulana ya kukata mikono (singlet) kwenye bwalo la chakula.
   - Hairuhusiwi mwanafunzi kuja na nguo zisizokuwa za shule.
   - Pia haruhusiwi kutumia “chombo chochote cha umeme.

3. Atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma.

4. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali.

5. Mwanafunzi asipige kelele anapokuwa darasani, kwenye ‘prep’, mazingira ya shule na katika mkusanyiko wowote.

6. LAZIMA mwanafunzi AWAHI NA AHUDHURIE mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.

7. NI LAZIMA Mwanafunzi awe katika sare ya shule kwa nyakati zifuatazo:- (a) Anapohudhuria masomo darasani.
   (b) Anapotoka nje ya shule kwa ruksa maalumu kwa shughuli yoyote itakayomlazimu kwenda nje ya shule.

8. NI LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (Pasi) cha maandishi.
9. Mwanafunzi lazima awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa/kulala (lights out) saa 5.30 usiku.
10. Mwanafunzi haruhusiwi:-
    (a) Kwenda kwenye nyumba za watumishi wa shule bila kibali maalum.
    (b) Kuingia kwenye Ofisi za Shule – Ofisi za walimu, jikoni, na maabara bila ruhusa.

11. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Mahudhurio hafifu darasani.
2. Wizi.
3. Kufuga ndevu.
4. Uasherati, ubakaji na ushoga/kuoa au kuolewa.
5. Ulevi na utumiaji wa madawa ya kulevya/uvutaji sigara.
6. Makosa ya jinai (Criminal Offences).
7. Kupigana au kumpiga mtu mwingine.
8. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi .
9. Kudharau Bendera ya Taifa.
10. Kupata au kutoa mimba/kusababisha mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
12. Kukataa adhabu halali.
13. Utoro
14. **Kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, "earphones" pamoja na redio**
15. Kujiachisha shule mwenyewe.
16. Kufanya jaribio lolote la kujiua/kutishia kujiua mfano kunywa sumu 17.
17. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi/walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
18. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
19. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
20. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

K. M. MILLONGO
MKUU WA SHULE
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BAGAMOYO
S.L. P. 42
BAGAMOYO

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. i) Jina kamili la mwanafunzi……Me/Ke
   ii) Tarehe ya kuzaliwa…….. mwezi……mwaka……..……...
   iii) Shule uliyotoka kidato cha Nne;……
2. Je wazazi wote wapo hai? Ndiyo / hapana…….…….…….
   a) Na kama hapana nani yuko hai ……
   b) Jina la mzazi (wazazi)…….…….
      Kazi yake: ……..
      Anuani yake: ……..……..
      Makazi yake : ……Simu:……

   c) Kama unalelewa na mlezi asiye mzazi wako;
      Jina la mlezi wako (majina matatu)……
      Uhusiano na mlezi wako (kaka,dada,n.k)…….……
      Kazi yake……..
      Anwani yake……..……..
      Makazi yake: …….Simu……..

3. Afya.
   a) Je una ulemavu wa viungo? Ndiyo./hapana……..……..
   b) Kama ndiyo taja aina ya ulemavu…….…….

4. Orodhesha majina ya ndugu watatu (nje ya uliowataja hapo juu) ambao wanaweza kuitwa kwa dharura.

	Jina	Uhusiano	simu
1.	……..	…….	……
2.	……..	…….	……
3.	…….	…….	…….

5. Uthibitisho wa taarifa iliyotolewa;
   Mimi (jina la mwanafunzi) ……..nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni ya KWELI na endapo itathibitika kuwa nimedanganya hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.
   Tarehe……..…….. Sahihi……..…….……..

6 Jina na sahihi ya mzazi/mlezi

Jina…….…… Sahihi…….……

7. Jina na sahihi ya mwenyekiti wa kijiji/Afisa Mtendaji/serikali za mitaa/kitongoji

Jina…… Sahihi…….. Muhuri……

AHADI YA KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi……..…….
Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **Shule ya Sekondari Bagamoyo kidato cha tano** mchepuo….
…….mwaka……ninaipokea na kuikubali nafasi niliyopewa.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili yangu binafsi, familia yangu na Taifa langu la Tanzania.

Ninaamini kuwa vitendo vyovyote vinavyosababisha uzembe katika kufanikisha
Makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, Shule yangu na familiya yangu na kwangu pia.

Hivyo ninaahidi kuwa;

1 Nitasoma kwa bidii na kufanya mitihani na majaribio yote ili kufikia malengo ya kufanya vizuri katika masomo.

2. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zinatolewa mara kwa mara.

3. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapa shuleni na nje ya shule.

4. Ikiwa nitakiuka sheria , kanuni, na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za shule.

Sahihi ya mwanafunzi: ……..Tarehe: ……

Sehemu ya mzazi/mlezi.

Mimi…….ninakubali mtoto wangu……
Kupata na kupokea nafasi katika shule ya Sekondari Bagamoyo kidato cha tano mwaka 2019/2020. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.

Anwani yangu ya kudumu ni……
……..
……..
Namba ya simu…….

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

Sahihi: …….tarehe:…….

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PART A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To: The Medical Officer (*Government Hospital)* From: Bagamoyo Secondary School,

…….. P.O. Box 42, ……. **Bagamoyo.**

……. **Date:……**

Mr/Mrs/Miss……. (Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time Secondary Education. The examination should include the following ineligible in case of a defect. Pregnancy (Category IV) will also render a girl candidate ineligible for a Secondary Education.

1. (a) Eye sight (b) Speech (c) Hearing (d) Limbs (e) Venereal Diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy.
2. Neuroses 3. Other Serious diseases.

Part B: **MEDICAL CERTIFICATE:**

1. (a) Eye sight:……. ……..…….
   (b) Hearing:…… ……..…….
   (c) Speech: ……. ……..…….
   (d) Limbs: …… ……..……..
   (e) Venereal Diseases: ……..……..
   (f) Leprosy:…….. ……..……
   (g) Epilepsy:……. ……..
   (h) TB: ……. ……...
2. Neuroses:……. ……..……..
3. Pregnancy:….. ……..……..
4. Other serious diseases: ……..……

   ……..…… ……

I have examined the above named, and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for fulltime Secondary Education.

Designation:…… …….. Date…….

Signature & official Stamp:

(To be completed by a Government Officer)

N.B: Incase of any serious health problem (s), the records from the Government Hospital MUST be submitted to School when reporting.

VIFUATAVYO NI BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI

Mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu kulingana na masomo yake.

MATHS& BAM	HISTORY	ACCOUNTANCY	COMMERCE	GENERAL STUDIES	GEOGRAPHY
1. Pure Mathematics 1, by J.K. Backhouse 2. Introductory Statistics, by A.M Plews. 3. Pure Mathematics 2, by J.K. Backhouse 3. Basic applied mathematics form 5 & 6 by Sillem Septine	1. History of Africa vol 1, by Okot B 2. A History of Modern Europe, by H.L Peacock 3. Mastering Modern World, by Norman Lowe 4. Major Events in Africa History, by Kamara 5. Major Issues in Africa History, by TIE. 6. History of Africa volume 2, by Okot B	1. Business Accountancy 11th edition by Frank wood Volume 2. 2. Business Accountancy 11th edition by Frank wood volume 2. 3. Accounting Manual Volume 1 4. Accounting Manual Volume 2 5. Simplified Accounting by Saleeme	1. Commerce simplified, by N.A Saleeme 2. Commerce its Theory and Practice, by Eveln Thomas 3. Principle of Marketing 3rd edition, by Philip Kotler	1. General studies for Advance level form **5,** by R.F Richard et Al 2. General studies for Advance level form **6,** by R.F Richard et al	1. Fundamentals of Practical Geography 2. Physical Geography, By Monkhouse 3. Geography in Diagrams, (Burnet 4. Practical Geography for Africa, by John 5. Human Economic Geography, by David Waugh 6. Human and Economic Geography, by Gilian C. Morgan 7. Integrated Geography Approach, by David Waugh. 8. Research Methodology:, C.R. Kothari, 2009, New Age International (P) Ltd, 2004, Second Edition

BIOLOGY	KISWAHILI	ECONOMICS	ENGLISH	CHEMISTRY	PHYSICS
1.Biological science(D) Taylor,N.Green	1.Kamusi sanifu (TUKI), 2.vuta nikuvute	1.Text Book of Economy (By J.L Hamson)	1.English language form five and six by Asheli	1.Essential physical chemistry by chand et al	1.Principle of physics by chand class xi and xii
2.Advanced Biology,(By C.J.Cleggy)	3.Rwanda magere 4. Kwenye ukingo wa Thim	2.Modern Economics	2.English language for form 5 and 6 by oxford	2.Conceptual chemistry by chand	2. A Level physics by Roger Muncaster
3.New understanding Biology (Glenn and Susan Toole	5. Usiku utakapo kucha 6.Morani 7.Kivuli kinaishi	3.Economics simplified by (N.A.Saleem)	3.A Man of the people by Chinua Achebe	3.Advanced chemistry by Cambridge press	3.Advanced physics by Nelkon
			4.University grammar of English 5.A Beautiful one's are not yet born by Ay kwei Arhmah 6.Betrayal in the city By Francis Imbunga	4.Physical chemistry by Mkayula et al Mzumbe bk project 5.Organic part A and B By Mzumbe bk project 6.In organic part 1 &2 , by TIE	4.Modern's ABC Physics for class XI &XII PART 1&2 By Satish K Gupta
			7.An enermy of the people By Henry Ipsen 8.Selected poems By TIE		